# Usalama wa Safari na Sikukuu

Sikukuu ni wakati wa mwaka wa furaha. Pia, ni wakati ambao watu wanapaswa kuchukua tahadhali ya uwezekano wa kutokea wa uhalifu.  Kuchukua tahadhari rahisi kunaweza kuhakikisha msimu wa sikukuu unakuwa salama na wa furaha.

## Kuandaa Nyumba Yako

### Taa

- Weka taa kwenye milango yote ya nje. Washa taa usiku kucha – zingatia kutumia vitambuzi vya jioni hadi alfajiri.
- Tumia vipima muda kwenye taa ili kutoa hisia kwamba uko nyumbani.

### Kusawazisha Mandhari

- Kata miti kwa urefu wa futi sita.
- Punguza urefu wa ua wa miti iliyooteshwa hadi futi tatu.
- Hakikisha mandhari ya milangoni na madirishani yamesawazishwa ili kuondoa mahali pa kujificha.

### Milango na Madirisha

- Hakikisha milango na madirisha yamefungwa.
- Hakikisha milango ya nje na mlango unaotoka karakana kuja nyumbani umetengenezwa madhubuti au wa chuma.
- Funga mlango wa karakana kwa kufuli; zingatia kuzima kifungua mlango wa karakana unapokuwa mbali.
- Usionyeshe zawadi yote dirishani au mahali ambapo zinaweza kuonekana kutoka nje ya makazi.

### Vidokezo

- Tunza vitu vya thamani, kama vile vito, silaha za moto na hati zenye utambulisho binafsi kwenye sefu.
- Usifiche ufunguo nje hata mara moja.
- Fikiria kuajiri mhudumu wa nyumba unapokuwa mbali.
- Waombe majirani wakusaidie kukusanya takataka na mapipa ya takataka na magazeti.
- Vunja masanduku kabla ya kuyaweka kwa ajili ya kuyarejeleza.

## Ununuzi, Kusafiri, na Mtandaoni

- Egesha gari katika eneo lenye mwanga wa kutosha, lifunge gari lako na pandisha vioo vya madirisha.  Hifadhi vifurushi mahali ambapo haviwezi kuonekana.
- Epuka kubeba kiasi kikubwa cha pesa taslimu, lipa kwa kutumia kadi ya benki au ya mkopo.
- Epuka kuvaa nguo au vito vya bei kubwa.
- Jihadhali na mazingira yako, amini hisia zako.
- Usinunue zaidi ya unachoweza kubeba; muombe msaada rafiki au mfanyakazi wa duka.
- Jihadharini na aina yoyote ya wakala mlangoni – wahalifu wakati mwingine hujifanya kama tarishi au wanatafuta michango.
- Hifadhi risiti zote; anzisha faili ili kukusaidia katika kulinganisha taarifa za benki za sikukuu na/au za safari.
- Tumia tovuti salama kwa ununuzi.  Tazama "https" kwenye URL au kufuli iliyofungwa chini ya ukurasa huo.
- Chapisha na uhifadhi uthibitishaji wote wa ununuzi wa mtandaoni.
- Fuatilia vifurushi kupitia tovuti ya usafirishaji.
- Safirisha vifurushi vinavyohitaji sahihi.
- Ruhusu vifurushi vipokelewe na rafiki, ndugu, jirani au mwajiri.